# 16 Siku za Uanaharakati 2024

## Uwajibikaji, Rasilimali, na Maazimio.

## Muhtasari wa Kampeni

## Utangulizi

Kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ni tukio la kidunia ambalo limekuwa likiandaliwa toka mwaka 1991 ili kuhamasisha usalama wa wanawake na haki ya kuishi bila unyanyasaji. Kampeni hii hufanyika kila mwaka kuanzia tarehe 25 Novemba hadi Desemba 10, huanza Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na kumalizika na Siku ya haki za Binadamu. Mtandao wa Kuzuia UWAKI unaongoza juhudi za kikanda katika Pembe ya, Mashariki, na Kusini mwa Afrika kwa kutumia kiti ya utetezi na kuchukua hatua kwa takribani miaka 20.

Kampeni ya mwaka huu inaangazia maadhimisho yajayo ya miaka 30 ya jukwaa la kuchukua hatua la Beijing , ambalo lilipitishwa mnamo mwaka 1995 katika Mkutano wa Nne wa Dunia wa Wanawake. Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing ni hati inayoweka alama muhimu ya kihistoria ya haki za wanawake duniani, ambapo viongozi wa dunia waliazimia kuendeleza mapendekezo ya kimkakati na hatua katika maeneo 12 mahususi, ikiwa ni pamoja na Ukatili dhidi ya Wanawake. Mwaka huu, tunawaalika watia saini wa jukwaa la kuchukua hatua la Beijing na wadau ili kuazimia upya katika vipaumbele hivi, kuendeleza na kutekeleza taratibu za uwajibikaji katika kutathmini maendeleo yao, na kutoa rasilimali zinazohitajika ili kuimarisha kazi hii. Kampeni yetu inasisitiza kuhusu kuchukua hatua za haraka katika kukomesha aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na wasichana, na inatoa wito wa uwepo wa sera thabiti, ufahamu mkubwa, na hatua madhubuti za wadau wote katika kulinda haki zao na kuhakikisha usalama wao duniani kote.

Raising Voices

16 DAYS

GBV PREVENTION NETWORK
Building Momentum•Fostering Activism

# Kupendekeza kwa mara nyingine Maazimio ya Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake kupitia Mifumo bora ya Uwajibikaji na yenye Rasilimali za kutosha.

Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing linasisitiza wajibu wa serikali wa kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake kupitia uundwaji wa mifumo thabiti ya uwajibikaji. Juhudi za uwajibikaji zilizoainishwa katika jukwaa la kuchukua hatua la Beijing ni pamoja na kuunda na kutekeleza sheria zinazoharamisha ukatili wa kijinsia, kuhakikisha kwamba vyombo vya usalama vya serikali kama vile polisi na vikosi vya usalama wanawajibishwa wanapofanya Ukatili Dhidi ya Wanawake, na kujenga Mifumo ya haki kwa wahanga wa unyanyasaji katika kutafuta msaada wa kisheria. Jukwaa pia lilisisitiza umuhimu wa utaratibu mzuri wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa ili kutathmini maendeleo na kutambua maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa.

Kwanyongeza, Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing linaangazia umuhimu wa rasilimali za kutosha ili kukomesha kikamilifu ukatili dhidi ya wanawake, ikiwa ni pamoja kuwepo na ufadhili wa huduma za kina za wahanga kama vile usaidizi wa kisheria, huduma za afya, nyumba salama na usaidizi wa kisaikolojia. Jukwaa linahimiza nchi kufadhili elimu kwa umma ambayo inabadilisha mitazamo na tabia zinazokumbatia ukatili na kutekeleza programu za mafunzo kwa wataalamu wanaofanya kazi ya kutoa huduma kwa wahanga. Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing linahimiza nchi kutenga rasilimali kupitia bajeti ya serikali ili kutekeleza mipango ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Tangu hati hii ya kihistoria ilipotiwa saini kwa kipindi cha takribani miaka 30 iliyopita, mazingira ya kushughulikia Ukatili Dhidi ya Wanawake yamebadilika sana. Katika muongo uliopita, tumekusanya ushahidi unaoonyesha kwamba inawezekana kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake kupitia programu za mabadiliko ya kijinsia. Nchi nyingi zimetunga sheria zinazoharamisha ukatili wa kijinsia, na kutoa misingi wa haki na uwajibishwaji wa wanaofanya vitendo vya ukatili. Upatikanaji wa huduma kama vile nyumba salama, simu za dharura, na usaidizi wa kisheria umeongezeka, na kutoa usaidizi muhimu kwa wahanga wa ukatili. Tumeona pia ongezeko la idadi ya watendaji ambao wanashughulikia suala la Ukatili dhidi ya wanawake ndani na katika sekta mbalimbali. Tunajua kwamba mabadiliko tunayoyataka lazima yaongozwe kwa kupitia utaalamu wa mashirika ya haki za wanawake katika nchi husika, yenye ufadhili unaonyumbulika, wa miaka mingi unaojenga jamii yenye haki zaidi.

Hata hivyo, changamoto zinaendelea Kuongezeka kutokana na utawala wa kimabavu unaendelea kote duniani ambao umesababisha kuenea kwa mipango ya kupinga masuala ya jinsia ambao unalenga kurudisha nyuma maendeleo tuliyofikia. Ushinikizaji na utekelezaji usio thabiti wa sheria, ukiambatana na ufadhili usiotosheleza kwa programu na huduma, unadhoofisha juhudi za kuwalinda wanawake ipasavyo. Kanda nyingi bado hazina utaratibu maalum wa kukusanya takwimu, hivyo inakuwa ni vigumu kuelewa ukubwa wa tatizo la ukatili

dhidi ya wanawake na kushindwa kupima maendeleo tuliyofikia. Kanuni za kitamaduni na kijamii zilizo jikita kwenye jamii zinaendelea kusababisha ukosefu wa usawa wa kijinsia na unyanyasaji, na kuweka vikwazo vinavyozuia wanawake kutafuta msaada au kutoa taarifa za unyanyasaji. Mashirika ya haki za wanawake na vuguvugu za kifeministi bado zinapata ufadhili kidogo kutoka kwa wafadhili ambao kwa muda mrefu hawataki kuwepo na usawa wa mamlaka kati yao nawale wanaowafadhili. Ili kuondoa kabisa ukatili dhidi ya wanawake, kunahitajika kuwekwa ahadi mpya ili kuhakikisha utekelezaji thabiti, ufadhili wa kutosha, takwimu za kina, na imani isiyozuiliwa ya mamlaka katika vuguvugu la kifeministi.

Kwa hivyo, tunasimama katika kampeni ya kimataifa ya Siku 16 ili kuwahimiza wadau kuimarisha juhudi zao za kuondoa Ukatili Dhidi ya Wanawake. Tunahitaji mipango madhubuti kutoka kwa serikali ili kutimiza ahadi walizotoa miaka 30 iliyopita: kutekeleza sera zinazozuia na kukabiliana na unyanyasaji, kutoa ufadhili wa kutosha kusaidia juhudi zisizo za kiserikali, kuimarisha juhudi zinazolenga kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, kwa wanawake katika hali zote, ikiwa ni pamoja na wahamiaji, wanawake wenye ulemavu, wanawake wenye umri mdogo, na wanawake wenye hisia mbalimbali, miongoni mwa wengine, na hatimaye kujenga dunia ambayo wanawake na wasichana wote wanaweza kuishi bila ya ukatili.

# Malengo Ya Kampeni

Kupendekeza kwa mara nyingine azimio kwenye Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing lenye jukumu la kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na wasichana na kuandaa mifumo ya uwajibukaji na rasilimali zinazohakikisha ufanisi katika kuzuia, kulinda na kukabiliana na aina zote za ukatili dhidi ya wanawake.

## Watu binafsi

Kila mtu ajenge tabia ya uwajibikaji na kuzungumza kwa uwazi juu ya ukatili, kusaidia waathirika, na kila mmoja ajielimishe mwenyewe na kuelimisha wengine juu ya ahadi zilizotolewa za kukomesha ukatili dhidi ya wanawake na wasichana katika Jukwaa la kuchukua hatua la Beijing.

## Mashirika

Yashirikiane na mashirika ya kifeministi ili kupaza sauti na kupewa ufadhili katika kazi zao muhimu, kukusanya rasilimali na utaalam ili kusukuma mabadiliko ya kimfumo katika viwango vya jamii, taifa na kimataifa.

## Jamii

Kuandaa sehemu salama ambapo waathirika wanaweza kupata usaidizi bila unyanyapaa, na washirikiane na mashirika ya wanawake wa eneo husika ili kupinga kanuni hatari za kijamii zinazoendeleza ukatili dhidi ya wanawake.

## Serikali

Kuimarisha na kutekeleza mifumo ya uwajibikaji ya kufuatilia, kutekeleza, na kutoa taarifa kuhusu sheria na sera za kupinga ukatili, huku zikitenga rasilimali za kutosha kusaidia huduma kamilifu za waathirika na juhudi za kuzuia.